

## **Maswali**

1. Nani alimwonea Yesu wivu?
2. Walipanga kufanya nini?
3. Walipeleka Yesu kwa nani?
4. Maaskari walimfanyaje Yesu?
5. Yesu aliomba nini kwa Mungu?
6. Ni vipi Yesu alionyesha upendo kwa mamake?
7. Anwani juu ya msalaba ilisema nini?
8. Nani alimzika Yesu, na alimzika wapi?
9. Nini ilifanyika siku ya tatu?
10. Nini ilifurahisha wanawake na wanafunzi?
11. Yesu angali hai?

## **Majibu**

1. Watawala walimwonea Yesu wivu.
2. Walipanga kumuua.
3. Walimpeleka Yesu kwa Pilato mtawala wa Rumi.
4. Maaskari walimpigilia Yesu kwa msalaba wa mbao katikati ya wezi.
5. Yesu aliwaombea msamaha kwa Mungu.
6. Yesu aliuliza mwanafunzi mmoja amtunze mamake.
7. MFALME WA WAYAHUDI.
8. Rafiki wa Yesu alimzika kwa pango lilokuwa bustani.
9. Mungu aliwatuma Malaika waviringishe jiwe litoke na kufanya Yesu awe hai tena.
10. Walifurahi kwa kuwa Yesu alikuwa hai tena.
11. Ndiyo, Yesu yu hai milele na milele.

## **SHULE YA JUMAPILI YA CBM**



**Awamu ya 1 Mwaka wa 1**

# **45 Yesu alikuwa na akawa hai tena**

## **Marejeo**

Marko 15:21-47 na Marko 16

## **Kiini cha somo**

Kuonyesha upendo wa Yesu aliyekufa kwa ajili ya dhambi zetu na kufufuka kwake ni furaha yetu

## **Maneno maalum**

1. Wivu wa watawala + panga kuua + uongo mbaya.
2. Pilato + lazima afe + askari + msalaba + samahe.
3. Maria ahuzunika + wanafunzi kujiadhari.
4. Kufa + MFALME WA WAYAHUDI.
5. Rafiki + chukuwa mwili + kunja + pango + jiwe kubwa.
6. Siku ya tatu + malaika + Yesu yu hai.
7. Wanawake + manukato + malaika + Yesu yu hai + furahi sana.


**45.1** Yesu kila wakati alikuwa anajitahidi sana kuwafundisha watu wampende Mungu na wapendane pia. Aliwafundisha kuhusu Ufalme ya Mungu ambao atakaporudi atauweka hapa duniani. Naye Yesu ndiye atakuwa Mfalme wa huo Ufalme. Watu wengi sana walimpenda Yesu na pia walipenda kusikiliza maneno yake. Lakini watawala waliopaswa kuwafundisha watu kama vile Yesu alivyokuwa akifundisha, wakamwonea Yesu vivu kwa sababu watu walipenda kumsikiliza badala ya kuwasikiliza wao.

Pia Yesu aliwasaidia wagonjwa kwa kuwaponya, na hata kuwafufua watu waliokuwa wamekufa. Masikini walimpenda Yesu, lakini watawala wakafikiria kuwa kamwe hawatapata watu wa kuwasikiliza tena, wakati Yesu akiwa angali anaishi. Kwa hiyo wakafanya shauri la kumwua Yesu. Yesu hakuwa amefanya kosa lolote, lakini baadhi ya watu waovu waliamua kumsingizia maneno ya uongo kuwa ndiye aliyesema.

**45.2** Ndipo wakampeleka Yesu kwa Pilato, ambaye alikuwa ni mtawala wa Rumi. Na Pilato akasema kuwa Yesu ni lazima afe. Kwa hiyo maaskari wakampeleka hadi kwenye mlima nje ya mji wa Yerusalemu.

Walimweka Yesu juu ya msalaba ili afe pamoja na wahalifu wawili ambao waliwekwa mmoja mkono wake wa kushoto na mwingine mkono wake wa kulia. Hapo ndipo alionyesha jinsi alikuwa mtu shupavu na jasiri. Alifahamu walilolitaka watawala

na maaskari – kumuumiza tu. Hata hivyo aliwasamehe. Katika sala yake aliwaombea kwa Mungu akisema, "Baba wasamehe dhambi zao maana hawajui walitendalo."



**45.3** Kisha Yesu akamwangalia mama yake na wenzake waliokuwa wamesimama karibu. Alifikiria jinsi mama yake atakavyokuwa na huzuni sana, kwa hiyo akamwambia mmoja wa wanafunzi ili amtunze kama vile ndiye mama yake hasa. Na akamwambia amtunze, ili asijisikie upweke na kuwa na huzuni.

**45.4** Na hatimaye Yesu akafariki, na anwani juu ya msalaba yenye maandishi haya: "**MFALME WA WAYAHUDI**". Watu hawakuamini kama itakuwa kweli, lakini tunafahamu kabisa kuwa Yesu atakuwa Mfalme wa Ufalme wa Mungu.

**45.5** Rafiki wa Yesu akauchukua mwili wake na kuupaka manukato kisha akauweka mwili wake ndani ya sanda ya kitani safi na kumzika ndani ya kaburi ambalo mtu hajazikwa ndani yake karibu sana na bustani. Kisha akavingirisha jiwe penye mlango wa kaburi.

**45.6** Siku ya tatu Mungu alituma malaika wake kwenda kumfufua Yesu. Wakarivingirisha jiwe pale penye kaburi na wakamfufua Yesu.

**45.7** Na baadhi ya wanawake walikwenda kaburini alfajiri na mapema ili kuupaka manukato mwili wa Yesu. Ni mshangao ulioje waliokuwanao walipokuta jiwe lilokuwa limewekwa pale kaburini likiwa limeodolewa penye mlango wa kaburi. Malaika wakawaambia, Msiogope. Yesu yu hai. "Enendeni mkawaambie wanafunzi habari hii njema"

Ndipo wanawake walipokwenda mbio kuwajulisha mitume. Ilikuwa ni habari njema ilioyojo! Jinsi walivokuwa na mshangao kubwa waliposikia kuwa Yesu yu hai tena! Yesu akaenda kuongea na rafiki zake na wote wakafurahi sana kwa kuwa Mungu alikuwa amemfufua Yesu yu hai milele na milele. Hii bado ni habari njema tena ya kushangaza. Na inatupatia sisi furaha pia.